

MWAMANGA AAGWA RASMI TASAF

Kamati ya Taifa ya Uongozi ya Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Jamii TASAF, Menejimenti, Wafanyakazi pamoja na wadau wa Mfuko wa Mfuko wameshiriki hafla maalum ya kumuaga rasmi Mkurugenzi Mtendaji Mstaafu wa Taasisi hiyo Bwana Ladislaus Mwamanga iliyofanyika jijini Dar es Salaam 6 Agosti 2023.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo ya kumuaga Bwana Mwamanga ambaye amefanya kazi TASAF kwa miaka 23 katika nyadhifa tofauti. Alianza kama Mtaalau wa Teknolojia ya habari, akawa meneja wa kujenga uwezo na kumaliza kama mkurugenzi Mtendaji- alikuwa ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete ambaye katika hotuba yake alisifu utendaji kazi wa Bwana Mwamanga katika kuhakikisha malengo ya Serikali ya kuzinusuru kaya masikini unafikiwa.

Mhe. Kikwete alisema Serikali itatumia huduma ya Bw. Mwamanga katika maeneo mbalimbali licha ya kuwa amestaafu.

“Mwamanga umetuachia TASAF ambayo imekuwa mkombozi kwa wananchi, nimepata kuzunguka katika maeneo mbalimbali na kushuhudia simulizi na hadithi kuhusu mpango huu za mafanikio na changamoto zake. Miaka 23 ya utumishi wako imekuwa ya mafanikio,” alisema Kikwete.

Akitoa salamu za shukrani kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Salhina Mwita Ameir amemsifu Mwamanga kwa kuwa sehemu ya mafanikio ya TASAF Zanzibar, na kwamba kazi na alama aliyoiacha vitaendelea kudumu.

“Mwamanga ni mtu wa watu ndiyo maana hata Zanzibar tulimwandalia hafla ya kumuaga kutokana na utendaji wake. Tumefanya kazi na Mwamanga kwa ushirikiano mkubwa na amekuwa mfano katika TASAF hasa Zanzibar”. Alisema Ameir.

Kwa upande wake, Bwana Mwamanga alimshukuru Mhe. Rais pamoja Serikali kwa kumuamini, lakini pia akawashuru viongozi na wafanyakazi wa TASAF kwa ushirikiano ambao ulimfanya awe miongoni mwa mafanikio ya mfuko.

“Naondoka nimemaliza muda wangu, lakini nina uhakika nimeacha timu imara itakayoendeleza TASAF kwa sababu shughuli zote zilizofanyika zilikuwa za ushirikishwaji wa kutosha na baraka za viongozi wa juu wa Tanzania na Zanzibar.” Alisema Bw. Mwamanga

“Nikiwa nipo nje, basi misingi ya ushirikishwaji, kupendana, kufanya kazi pamoja, uwazi iendeleo, lakini tukianza kujenga ubinafsi hatufika huko. Hii programu (Tasaf) ipo kila kijiji, lazima kila mmoja awe na heshima kwa nafasi yake kwa ushirikiano,” aliongeza Mwamanga

Mwamanga pia alisema msingi wa shughuli za TASAF ni ushirikishaji wa wananchi kuanzia ngazi ya chini ambapo kunakuwa na uwazi ambalo ni jambo muhimu katika mchakato huo.

Aidha, amewasahi watumishi waliobaki kuendelea kuchapa kazi, kwa ushirikiano ili kuendeleza jitihada za serikali za kuwakomboa kiuchumi Watanzania.

“Tuendeleo kufanya kazi kwa bidii timu ya menejimenti na wafanyakazi tutoe ushirikiano na kuwa maadili mema. Tuheshimu kila mmoja katika maeneo ya kazi,” alisema Mwamanga.